# UQAB
Jarida la



Toleo 35 - Rabi-ul-Thani 1441 H / Disemba 2019 Miladi

**Kongamano baina ya Afrika na Urusi**

**Vita Dhidi ya Madawa ya Kulevya**

**Mpango wa Kupambana na Misimamo Mikali**

**Uharibifu Mkubwa dhidi ya Familia Sehemu ya 1**

**Uharibifu Mkubwa dhidi ya Familia Sehemu ya 2**

**SWALI/JAWABU: Ni Upi Uhalisia wa Mzozo wa Kimataifa na Ushawishi wake ndani ya Algeria?**




## CEDAW ni Uhalifu wa Karne dhidi ya Mwanamke Muislamu

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

# Kampeni ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir: #WaacheniHuruDadaZetu #MwacheniHuruDadaRomana #MwacheniHuruDktRoshan

Kafiri Mmagharibi kwa makusudi anaendelea tokea hapo awali hadi sasa ili kuvunja familia, mujtma na Ummah wa Waislamu wote na kulichukua suala la mwanamke na kulitabban katika kueneza ustaarabu na fikra zao hususan katika nchi za Waislamu na kuelekeza vichwa vya habari muhimu na hatari ili kufikia ushindi dhidi ya vipengee vya Uislamu kama vile kubadilisha dini na kuleta maendeleo katika khutba za kidini na kubadilisha vipengee vya hukmu ili kuoana na madai yao ya usasa huku wakiilenga mishale yao ya sumu kuielekeza kwa wanawake Waislamu na jukumu lao msingi na stara yao ili kuhakikisha jukumu la muhimu katika maisha ya familia na mujtama. Hivyo basi, Umoja wa Mataifa ulitabban yote haya na kuzindua mikataba mingi na makongamano ya kimataifa kama vile Tangazo la Kuondosha Aina Zote za Unyanyasaji dhidi ya Wanawake (CEDAW) mnamo 1979, makubaliano hayo maovu ambayo yanayokaribiana katika uovu sawia na Tangazo la Balfour. Makubaliano juu ya "Kusitishwa kwa sheria na desturi pasina kuzingatia ni za dini na kuweka mahala pake sheria za kimataifa."

Hivyo basi, muendelezo wa makongamano ya kimataifa yalifanyika ili kuipa nguvu mikataba hiyo na kufanyakazi ili kuitekeleza na kuifaulisha. Kongamano la kwanza lilikuwa mnamo 1975, lililoitwa Mwaka wa Kimataifa wa Wanawake lililofanyika Mji wa Mexico, lililingania usawa, maendeleo na amani… Huu ulikuwa ni ulinganizi wa kiujanja ili kupatikane usawa baina ya wanawake na wanaume. Kampeni hii nia yake ni kuwaamsha Waislamu kwa ujumla na hususan wanawake Waislamu kuhusiana na hatari inayotokana na makubaliano hayo yaliyo na sumu hususan (Makubaliano juu ya Haki za Mtoto). Na hatari ya miungano ya wanawake ambayo inazunguka katika mzunguko wa Kafiri Mmagharibi mkoloni anayepigia debe thaqafa yake na fikra zake fisadi. Mwenyezi Mungu ni Muweza, wanapanga njama na Mwenyezi Mungu ni Mbora katika mipango.

**HASHTAG/MWITO WA KAMPENI**

#واديس_ضفرن
#WeRejectCEDAW



Email: info@uqab.or.ke

# HABARI & MAONI

# Kongamano baina ya Afrika na Urusi: Viongozi wa Kiafrika Wanaiuza Afrika kwa Madalali wa Kirasilimali




**Habari:**

Viongozi wa Serikali zaidi ya 40 wa nchi za Afrika walihudhuria Kongamano la kwanza baina ya Afrika na Urusi katika mji wa Sochi. Kongamano hilo la siku mbili 24 na 25 Oktoba 2019 liliandaliwa kwa pamoja na Rais Vladmin Putin na mwenzake rais wa Misri Abdel Fattah el-Sisi uliangazia zaidi masuala ya kibiashara baina ya Urusi na Afrika likiwemo pia suala la usalama. Kwenye mahojiano ya awali na shirika la habari la serikali la TASS siku ya Jumatatu, 21 Oktoba 2019, rais Putin alisema: "Mkutano huu wa siku mbili ni hatua ya kufufua tena mahusiano yake ya vita baridi ampapo mataifa ya Kiafrika yalijiunga na utawala wa Moscow kwenye vita vya kimfumo na Marekani hii ni kabla ya kusambaratika kwa muungano wa kisovieti ni tukio la kipekee na hatua msingi"

**Maoni:**

Mnamo Machi, 2014 Muungano wa Ulaya na mataifa kama Marekani, Canada, Australia, Japani, Uswizi, New Zealand, Iceland na mengine yalianza kuiwekea Urusi vikwazo vya kiuchumi kutokana na hatua yake ya kuiteka Crimea. Vikwazo hivyo viliathiri uchumi wa Urusi; taifa ambalo ni moja wapo ya mataifa yenye ushawishi mkubwa duniani. Kongamano hili bila shaka ni miongoni mwa juhudi zake za kuokoa uchumi wake ambao umekua kwa mwaka huu kwa asilimia 1 tu pekee kutoka asilimia 2.3 katika mwaka jana 2018. Mataifa makubwa yanapora rasilimali za Afrika kupitia kile kinachoitwa 'mikao ya maendeleo ya biashara' kama vile Jukwaa la Biashara baina ya Amerika na Afrika, Jukwaa la Ushirikiano baina ya Uchina na Afrika, Japan, Kongamano la Kimataifa la Tokyo la Maendeleo ya Afrika (TICAD) n.k. Licha ya kwamba Urusi inasafirisha bidhaa za vyakula kwa thamani ya dolari bilioni 25 na silaha za thamani ya dolari bilioni 1 kuingia Afrika, inakuwa ni sawa na one baharini ikilinganishwa na Uchina ambayo katika kubadilishana kwake bidhaa na Afrika imetia faida ya dolari bilioni 204! Kwa upande mwingine, biashara ya Urusi na Afrika iko kwa kiwango cha dolari bilioni 26! Hivyo basi, Moscow inalenga kupatiliza fursa ya kongamano hilo ili kuweka mpango wake wa kushindana na Amerika, Muungano wa Ulaya na Uchina kama washirika wa kimikakati ndani ya bara lililo na utajiri wa rasilimali.

Ni wazi sasa utawala wa Putin unaumezea mate utajiri wa Afrika na una matumaini ya kuongeza maradufu biashara yake. Kwa mujibu wa shirika la Habari la Serikali ni kwamba tayari kwenye mkutano huo Urusi na baadhi ya tawala za Kiafrika zimetia saini mikataba ya miradi kadhaa kama vile teknolojia ya nuklia, uchimbaji madini na viwanda. Kwa ujumla Urusi imetenga kitita cha dolari bilioni 190 za kuwekeza katika miundombinu inayotarajiwa kutoa faida ya dolari bilioni 7.

Moscow inawekeza katika utengezaji wa zana za kivita ikiwemo mradi wa nuklia ambao umekua ukionekana kuwa tishio dhidi ya Marekani. Hatua yake ya kuiuzia silaha Afrika ni jaribio lake la kuathiri siasa za Afrika ili iweze kupata baadhi ya vibaraka wake watakaofanikisha tamaa zake za kuipora Afrika. Hata hivyo kwa kuwa nchi nyingi barani Afrika bali karibu zote zimo katika ushawishi wa Marekani na Ulaya, jaribio lake hilo sio rahisi kufaulu hasa tukizingatia kuwa yuko nyuma kiuweledi wa kisiasa ukilinganisha na Marekani na Ulaya. Urusi ina kambi ya kijeshi huko Jamhuri ya Afrika ya

*Endelea Uk..4*

Kati, nchi inayotajwa kuwa na umuhimu mkubwa wa kistratejia na eneo salama baina ya Waislamu wa kaskazini na Wakristo wa kusini. Rwanda nchi ambayo inatajwa kuwa na mahusiano ya karibu na Urusi tayari baraza lake la mawaziri limeidhinisha kuasisiwa kwa kituo cha nuklia kufikia 2024.

Warasilimali kwa upande mmoja wanaupora utajiri wa Afrika kwa kisingizio cha kudumisha usalama, kuhifadhi na kulinda mazingira ya Afrika na kufutilia mbali madeni. Kwa upande mwingine viongozi wa Afrika chini ya bendera ya mipango ya maendeleo; viongozi wa Afrika wamekuwa madalali wakuiuza Afrika kwa madalali warasilimali wakubwa kwa kupewa mabaki kidogo ambayo yanaishilia kusababisha madhara zaidi kuliko mazuri kwa nchi zao na raia wao. Nchini Kenya kwa mfano, mradi wa SGR amabo ulidhaminiwa kwa mkopo wa bilioni Ksh324 umepelekea kufutwa kazi kwa asilimia 60 ya wafanyikazi katika Vituo vya Usafirishaji Makasha (CFS) kufuatia agizo la serikali la kusafirisha makasha yote yaliyowasili Mombasa kwenda Nairobi kupitia SGR badala ya barabara!

Afrika lazima itambue kwamba Urusi, Uchina, Marekani na Ulaya yote ni mataifa ya kibepari yanayong'ang'ania maslahi yake barani. Hivyo mikataba ya kibiashara kwa bara la Afrika si lolote ila ni kinyang'anyiro juu ya rasilimali zake. Mataifa hayo hutayarisha mazingira mwafaka ndani ya Afrika kupitia kuzunguka na kutambua utajri ulioko kwenye nchi kavu na bahari huku wakihonga viongozi wa Kiafrika, kuzidisha matumizi yao ya kijeshi barani kwa kile wakiitacho 'ujumbe wa kuweka Amani na kufanya ziara kadhaa za kiarais kwa nchi hizo kwa lengo tu la kupata utiifu wa kisiasa utakaowawezesha kuchukua mafuta na gesi. Makampuni makubwa ya kibepari pamoja na serikali za Kiafrika wao wote wanasoma kutoka katika ukurasa mmoja wa Urasilimali na hivyo basi utajiri unaozalikana na mauzo ya nje huzunguka tu miongoni mwao huku wakimuacha mlalahoi kwenye umasikini. Serikali pekee itakayolinda kikweli utajiri wa bara la Afrika lililobarikiwa ni Khilafah kupitia kukata kabisa ushirikiano na mataifa ya kirasilimali hivyo kuweza kuondosha taswira za kutamausha za bara hili za njaa, maradhi na kutojua kusoma na kuzibadilisha kuwa sura za siha, afya na maendeleo.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut TahrirKenya**

# Vita Dhidi ya Madawa ya Kulevya Havitafaulu chini ya Mfumo wa Kirasilimali

Mnamo Ijumaa, 18 Oktoba 2019, ripoti ya uchunguzi iliyopeperushwa na Runinga ya France 24 ilifichua kwamba Mji wa Mombasa umepatikana kuwa ndio kitovu cha usafirishaji wa madawa ya kulevya na ni njia ya heroin na cocaine kuelekea duniani. Miezi michache nyuma, Waziri wa Ndani na Mipango ya Serikali ya Kitaifa Fred Matiangi aliwaonya viongozi wa Pwani dhidi ya kuhusishwa na madawa ya kulevya. Onyo hilo ilitolewa baada ya magenge ya vijana waliobeba mapanga na kuwashambulia wakaazi wa Kaunti ya Mombasa na kuwajeruhi watu 14 hivyo kumpelekea Waziri kuanza upya vita dhidi ya madawa ya kulevya ndani ya mji wa Pwani. Katika hotuba yake alisema, "Litakuwa zoezi chungu lakini ninafuraha viongozi wa kisiasa wa eneo wamekubali kutunusuru. Nimejadiliana nao mikakati yetu na wameiridhia." Ili kuonekana kwamba anayafanyiakazi matamshi yake mnamo 13 Agosti 2019 vyombo vya habari viliripoti kwamba timu ya mjumuiko wa vikosi vya kupambana na madawa ya kulevya vilikuwa vimetoa ilani ya kumkamata na walitarajiwa kuvunja na kuingia katika nyumba ya mfanyibiashara wa Mombasa Ali Punjani kwa madai ya usafirishaji wa madawa ya kulevya.

Hakika, huku Kenya ikiwa ndio mfano wa kuzingatiwa, vita dhidi ya madawa ya kulevya havikuanza leo. Mnamo 2017, ndugu wawili waliodaiwa kuwa wakuu wa madawa ya kulevya walishikwa na kukabidhiwa mamlaka za Amerika ili kushtakiwa kwa mashtaka yanayohusiana na madawa ya kulevya. Na katika sherehe ya mwaka ya kilimo huko Mombasa katika mwaka wa 2015, kiongozi wa serikali alitangaza, "Sasa nina furaha kwamba vijana wako makini na wanaweza kufanyakazi… Vita sasa lazima viwe juu ya madawa ya kulevya," Tangazo hilo lilitolewa baada ya kushikwa na kuharibiwa kwa meli iliyoshukiwa kubeba heroin yenye thamani ya milioni Ksh28. Katika mwaka wa 2013, watawala wapya walioingia madarakani walitabban sera ya kuwafurusha wakuu wa madawa ya kulevya ambapo raia wa Nigeria alifurushwa haraka kwenda Nigeria na kusababisha mzozo wa kidiplomasia baina ya Kenya na Nigeria. Ama kuhusu mwaka 2012 ndani ya serikali ya muungano, ubalozi wa kigeni ulitoa ripoti kuhusu madawa ya kulevya na wakuu wa madawa ya kulevya ikiwahusisha wanasiasa tajika, wafanyibiashara na wanachama wa familia zilizoko uongozini. Waziri wa Usalama wa Ndani alitangaza uchunguzi kwa wale waliotajwa katika ripoti na kabla tu kutoa orodha hiyo bungeni, alipatikana amefariki kwa ajali ya ndege.

Hivyo basi kupitia mipango hii na mengine kama ya kubuni kitengo cha polisi cha kupambana na madawa ya kulevya ndani ya mataifa ya kirasilimali yameonekana yakitumia rasilimali na juhudi nyingi kupigana dhidi ya matumizi na usafirishaji wa madawa ya kulevya. Ama kuhusu uhalisia wa madawa ya kulevya, kwa mujibu wa ripoti ya Global Financial Integrity (GFI) iliyotolewa mnamo 27 Machi 2017 –soko ya dunia ya madawa ya kulevya ilikadiriwa kuwa kila mwaka ina thamani ya baina ya dolari bilioni 426 na dolari bilioni 652. Hivyo basi, ikiifanya kuwa ndio soko kubwa haramu lililotathminiwa baada ya lile la bidhaa ghushi. Hivyo basi kwa kuzingatia msingi wa kirasilimali unaosema kwamba, 'kitu chochote kinachovutia kina manufaa, na kitu chochote chenye manufaa ni kitu cha kiuchumi,' ni wazi kwamba kiwanda cha madawa ya kulevya kinayo thamani ya kiuchumi na hivyo basi itakuwa vigumu kupambana na kuipiga marufuku ndani ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali.

Kuhusiana na matunda ya madawa ya kulevya, kiongozi wa zamani wa afisi ya UN ya madawa ya kulevya na uhalifu, Antonio Maria Costa alisema, "baada ya kuanguka kwa soko la kifedha la dunia mnamo 20008, katika mifano mingi, fedha kutoka katika madawa ya kulevya ndio ilikuwa uwekezaji wa pekee wa kimitaji. Katika nusu ya pili ya 2008 mtaji ulikuwa ndio tatizo kuu la nidhamu ya benki na hivyo mtaji ukawa ndio kigezo muhimu," Napia akasema, "Mikopo baina ya benki ilidhaminiwa kwa fedha zilizotokana na madawa ya kulevya na amali nyingine haramu…kulikuwepo na ishara kwamba baadhi ya benki zilinusuriwa kupitia njia hiyo." Hivyo basi kwa mujibu wa matamshi ya afisaa mkuu wa UN, ni kimaumbile kukatikiwa kwamba matunda ya madawa ya kulevya yanacheza dori muhimu katika uchumi wa mataifa ya kirasilimali.

Kwa kufupisha tangu kutangazwa kwa vita dhidi ya madawa ya kulevya badala ya kuona kupunguzika kwa matumizi ya madawa ya kulevya kinyume chake ndio kinachotokea! Mnamo 1988 afisi ya UN ya madawa ya kulevya na uhalifu iliandaa kongamano lake la kwanza la kimataifa kuhusiana na madawa ya kulevya kwa kichwa, 'DUNIA HURU ISIYOKUWA NA MADAWA YA KULEVYA INAWEZEKANA'. Ni zaidi ya miongo mitatu tangu wakati huo na dunia bado haijakuwa huru kutokana na madawa ya kulevya. Haswa kinachoendelea tangu wakati huo ni kwamba dunia inakoloniwa na wakuu wa madawa ya kulevya. Felipe Calderon, mkuu wa serikali ya Mexico aliwahi kusema, "Kusitisha matumizi na usafirishaji wa madawa ya kulevya ni zoezi lilsilowezekana… naam lilikuwa sio lengo. Kwa vikosi vya polisi kusitisha kitu ambacho hakiwezekani kusitisha, ambacho ni matumizi na usafirishaji wa madawa ya kulevya."

Iko wazi kwamba mataifa ya kirasilimali yamefeli kusitisha janga la madawa ya kulevya kwa kuwa tokea mwanzo hawalioni kuwa ni janga. Ama kuhusu yale tunayoyaona kutoka kwa mataifa ya kirasilimali juu ya vita dhidi ya madawa ya kulevya na wakuu wa madawa ya kulevya, kiuhakika tutaendelea kuona filamu hizo kwa kuwa ni vitendo vya kiusanii vilivyo zinduliwa ili kuyadanganya macho ya wapiga kura kwamba kuna vita dhidi ya madawa ya kulevya. Ni wazi bila shaka kwamba lengo la vita dhidi ya wakuu wa madawa ya kulevya na matumizi ya madawa ya kulevya ni kupigana na washindani wa kibiashara pamoja na kudhibiti soko la madawa ya kulevya.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لاَ تُفْسِدُوا فِي الأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ

Na wanapo ambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Bali sisi ni watengenezaji."

**Khamis Mwangemi (Abu Leila)**

# Mpango wa Kupambana na Misimamo Mikali ni Sera ya Kuwagawanya na Kuwadhuru Waislamu

Maarufu duniani vinajulikana kama vita dhidi ya ugaidi, kampeni ya kijeshi ya kimataifa inayoongozwa na Marekani baada ya shambulizi la Semptemba 11, 2011 huko Marekani. Msamiati huu wa kampeni hutumia tasnifu tu ya vita (metaphor of war) kumaanisha mkusanyiko wa matendo mbalimbali ambayo kama ilivyofasiriwa tokea jadi matendo hayajumuishi vita maalum. Aliyekuwa rais wa Marekani G. W Bush, kwa mara ya kwanza alitumia msamiati huu wa vita dhidi ya Ugaidi mnamo Septemba 16, 2001 kisha akaurudia tena kuutaja kwenye hotuba yake aliyoitoa kwenye bunge la Congress. Na kwenye hotuba yake ya mwisho Bush akasema: "Adui wetu ni mtandao wa magaidi na kila serikali inayowaunga mkono." Ni wazi sasa Marekani imefeli katika oparesheni yake ya kutafuta inaowaita magaidi. Na ninani asiyejua kwamba Marekani yenyewe imekuwa na mtindo wa kutumia makundi iyaitayo yenye misimamo mikali katika mataifa mbalimbali kufikia kwenye maslahi yake. Kwa mfano, miaka ya themanini, Marekani alidhamini na kusaidia wapiganaji wa Kiafghanistan dhidi ya uliokuwa muungano wa nchi za Kisoviet. Yote haya inabainika kwamba Marekani kikweli sio mwenye kupambana na ugaidi bali vita vyake hivi ni ishara wazi ya unafiki wa wazi.

Rais Donald Trump tayari amekwisha hisi hasara kubwa ya vita ilivyopigana taifa lake huko Afghanistan, huku ripoti zikionesha kwamba Marekani amepoteza takriban dolari trilioni 1 na dolari bilioni 70 na wanajeshi wake zaidi ya 2400 kuuwawa. Isitoshe, gazeti la The New York Times lilichapisha habari chini ya anwani "Miongo miwili baada ya shambulizi la 9/11 Makundi ya wapiganaji ndio yameongezeka pakubwa." Habari hiyo ilielezea kuhusu utafiti wa Kituo kikuu cha kiutafiti Center For Strategic and International Studies (CSIS). Kituo hiki kipo Washington DC na hutumika kama nguzo muhimu sana katika sera ya kigeni ya Marekani. Kituo hicho kilitaja kwamba idadi ya makundi ya kipiganaji ya Kiislamu yanayopigana duniani imeongezeka kwa mara nne pindi serikali ya Marekani ilipoanza kupigana nayo baada ya tukio la Septemba 11. Ukiachilia mbali gharama ya takriban dolari trilioni 6 na wanajeshi takriban elfu 7 kupoteza maisha yao, hivyo ni wazi kuwa vita dhidi ya ugaidi vimefeli.

Pamoja na hasara kubwa iliyoipata na kupoteza askari wake, Marekani imeshindwa kihakika kuondosha makundi ya kipiganaji. Ni ishara wazi kuwa Marekani amepata hasara kubwa jambo ambalo hata watengezaji sera wake (Policymakers) wamelazimika kutangaza wazi kuwa vita vyake dhidi ya ugaidi vimefeli pakubwa. Lakini kwa kuwa 'ugaidi' ni kama jinamizi jipya analotumia katika kuupiga vita Uislamu kama mfumo kamili wa kimaisha kwa hivyo inaonekana Marekani inakuja na mikakati mipya kuupiga vita Uislamu chini ya kibandiko kipya cha: **'kupambana na misimamo mikali'**

Kutokea kwa msururu wa mashambulizi ya kigaidi duniani kote kumefanya Marekani na washirika wake kubuni misamiati mipya na mipango kadhaa. Misamiati kama vile: siasa kali (Radicalism) misimamo mikali (extremism) na itikadi kali (violent extremism). Sambamba na hayo, kumekuwa kukifanyika mikutano na semina mbalimbali kiulimwengu kuzungumzia suala la misimamo na itikadi kali na kuangazia juhudi za kimataifa zinazostahiki kufanywa ili kuzuia wenye kubeba itikadi kali na wanaowaunga mkono, kama vile wanaotoa mafunzo hayo, wanaosajili watu kujiunga na makundi ya kigaidi. Ukiachilia hayo mashirika mbalimbali ya kiserikali yameundwa kupambana na mafunzo ya misimamo mikali. Kwa mfano, Serikali ya Ufaransa, baada ya kushuhudia ndani yake msururu wa mashambulizi ikabuni mpango wa kitaifa wa kugundua na kuwatoa vijana "waliochanganyikiwa" kwenye misimamo mikali

Mwaka 2004 mipango ya Saudia kuwatoa vijana kwenye misimamo mikali ilianza pale ambapo waziri wa mambo ya ndani wa nchi hiyo akafanyia mabadiliko mkakati wa kupambana na ugaidi kwenda kuchukua hatua za kuimarisha usalama wa ndani kwa miundo ambayo itaangalia hasa kiini cha itikadi kali. Lakini cha ajabu, ni kuwa Saudia hiyo hiyo inayojizatiti kupambana na magaidi kwa upande mwingine imekuwa ikiaminika kushirikiana na mataifa katika ukanda wake kudhamini makundi ya kigaidi nchini Syria.

Mpango wa kupinga mafunzo ya itikadi kali hujulikana kama mikakati maalumu ya kupambana na ugaidi inayowalenga haswa wale wanaoaminika kuwa ni wabebaji itikadi kali na kuwa na misimamo mikali ya kidini au kisiasa kuwatoa kwenye misimamo hiyo wawe ni watu wenye misimamo ya kadri (moderate) na misimamo isiyokuwa mikali.

Tarehe 4 Juni, mwaka 2009, rais wa 44 wa Marekani Barack Obama akihutubia wanafunzi wa chuo kikuu cha Al-Azhar, Qairo Misri aliweka bayana kampeni ya Marekani ya kuushambulia Uislamu kimfumo chini ya kibandiko cha kupambana na itikadi kali katika chuo cha Azhar. Kwenye hotuba yake akasema: "Suala la kwanza tunalopaswa kukabiliana nalo ni suala la misimamo mikali kwa sampuli zake zote. Na nilipokuwa Mjini Ankara- Uturuki nikaweka wazi kwamba Amerika haina na wala kattu haitokuwa na vita na Uislamu. Hata hivyo tutapambana kidete na wenye kubeba itikadi kali ambayo ni tishio kubwa kwa usalama wetu…. kwa sababu tunakataa kilekile ambacho watu wa dini zote wanakikataa…kuwauwa wanaume na wanawake wasiokuwa na hatia". Mnamo 21 Mei, 2017, Donald Trump akaimarisha zaidi kampeni ya kuushambulia Uislamu pale alipofungua kituo cha kimataifa cha kupambana na misimamo mikali katika Mji wa Riyadh -Saudi Arabia. Ufunguzi wa kituo hicho kipya ulilenga kutoa taswira ya azimio kubwa la mataifa yaliyo na Waislamu wengi yawe kifua mbele katika kupambana na mafunzo ya misimamo mikali. 'Nataka nitoe shukrani zangu za dhati kwa mfalme Salman kwa uongozi wake imara kwa wanawake na watoto. Nami kama rais wa Marekani jukumu langu la kwanza ni kuwalinda Wamarekani.' Akasema Trump.

Kwa mtanziko (dilemma) huu wa ima kuungana na Marekani katika kampeni yake ya kuuhujumu Uislamu au kuwa na wale awaitao 'maadui', Waislamu wengi wameingia kwenye mtego wa Wamagharibi warasilimali wa kuuchukulia Uislamu kuwa ni Dini ya kiroho tu, na kwamba wale wote wenye kubeba ufahamu kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa kimaisha ulio na utatuzi wa kila kipengele maishani ikiwemo siasa hao ndio huitwa wenye itikadi kali kwani wanaufanya Uislamu kuwa mgumu! Waislamu hao wakawa sasa hawaoni uwajibu wa kupinga sera hizi mbovu za wamagharibi dhidi ya Uislamu na haja kubwa kwa wao kujadili kindani hizo fikra kama vile Jihadi

***Endelea Uk..7***

na Khilafah zinazoambiwa kuwa ni itikadi kali.

Baadhi ya Waislamu wanaona kuwa mpango ya kupinga mafunzo ya itikadi kali ni mpango mzuri kwa vijana wetu vilevile kwa Dini yetu huku wakiamini kuwa kuunga mkono mafunzo ya misimamo mikali ni kuunga mkono matendo ya ugaidi na vita. Wanavyuoni wakiserikali wakakubali mikakati ya 'kupambana na ugaidi' ama ile kampeni ya kupinga misimamo mikali na wanafanya juhudi wanavyuoni hao kuubadili Uislamu kwa kupinda maana ya sheria kadhaa za Uislamu ili zioane na fikra huria za kisekula. Kukatolewa fatwa za kiajabu na wanavyouni hao ambao kwa kusaka tonge wakipinga misimamo mikali na itikadi kali, bali wanashtumu matumizi ya matamshi kama vile Jihadi na Khilafah

Naam, kwa Waislamu kufanya hivyo inamaanisha tayari wametumbukia kwenye mtego uliotegwa na Wamagharibi ambao hudai na kutaka watu kuamini kwamba Uislamu ni kiini hasa cha utovu wa usalama duniani. Mbali na hayo muhimu kuelewa kuwa Uislamu ni mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt) ambapo sheria zake na maadili yake kattu haziwezi kubadilishika. Mwenyezi Mungu (swt) pekee ndiye aliye na mamlaka ya kuleta sheria na kuweka mipaka maalum ambayo Waislamu hawafai kuivuka. Hivyo, Marekani hastahiki kutungia Waislamu Uislamu mpya autakao yeye. Waislamu hawana khiyari ya kuchagua au kutochagua sheria za Mwenyezi Mungu (swt). Mtume (saw) ameeleza bayana kwenye Hadithi aliyoipokea Daruqutni pale aliposema:

إنَّ اللَّه تَعَالَى فَرَضَ فَرائِضَ فَلاَ تُضَيّعُوهَا، وحدَّ حُدُودًا فَلا تَعْتَدُوها، وحَرَّم أشْياءَ فَلا تَنْتَهِكُوها، وَسكَتَ عَنْ أشْياءَ رَحْمةً لَكُمْ غَيْرَ نِسْيانٍ فَلا تَبْحثُوا عَنْهَا حديثٌ حسن

'Hakika ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka, amekwisha faradhisha faradhi wala msizipuuze na akaweka mipaka wala msiivuke, na akaharamisha mambo wala msiyafanye na akanyamazia baadhi ya vitu iwe ni rahma kwenu pasina kuwa Yeye ni Mwenye kusahau basi msivitafiti.'

Mipango ya kupinga misimamo mikali ni mipango ya kimaonevu na kiuadui ambayo ni njama zinazolenga kuuhujumu Uislamu. Ni muhimu sana kufahamu kwamba matamshi haya itikadi kali au misimamo mikali yamejengewa maana pana sana kiasi cha uwezekano wa kutumika kiholelaholela hivyo kuunda mazingira yanayoruhusu Wamagharibi kuweka na kufuata sera chafu za kiuadui kama vile utumiaji wa mabavu wa kiserikali dhidi ya raia wa Kiislamu ili kuwalazimisha kubadili misimamo na Imani ya Dini yao. Wanavyuoni na Umma kwa ujumla wa Kiislamu wanapaswa kupinga sera hizi mbaya ambazo zimejengwa juu ya kuuzushia urongo Uislamu. Isitoshe hakuna mtu wa dini yeyote ile atakaye kubali mtu kando na dini yake ampe mafunzo yanayokinzana na Imani yake.

Uislamu haukubaliani na matendo ya fujo lakini ukweli wa kimakusudi wamagharibi wanaupinga na huweza kutumia yale mashambulizi yanayofanywa kuunasibisha Uislamu na ugaidi. Hata kama ni kweli kwamba kuna baadhi ya Waislamu au makundi yanayofanya mashambulizi lakini ukichunguza kwa makini vyombo vikuu vya habari kwa miaka mingi vimekuwa vikiyaelezea mashambulizi haya kwa kutia chumvi zaidi kuonesha Uislamu kuwa ni Dini iliyo na kiu cha kumwaga damu. Wakati huohuo vyombo hivyo vinaacha kueleza kwamba Waislamu wengi wamepoteza maisha yao kwenye mashambulizi hayo na kwamba jamii ya Kiislamu kwa ujumla wake imekuwa pia ikipinga matendo hayo kwa sababu yanapingana na Uislamu. Na ukaliaji wa kimabavu wa mataifa ya Kimagharibi katika nchi za Kiislamu na kupora mali za Waislamu ndio chanzo hasa cha hayo matendo wanayoyaita kuwa ni ugaidi.

Kwa kuwa sasa imebainikia wazi ulimwengu mzima kufeli kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa mfumo wa kibepari, Marekani inafanya juhudi kubwa kujaribu kuzuia kusimama kwa Uislamu kama mfumo mbadala ulio na uwezo wa kutatua matatizo ya kisiasa na kiuchumi yanayokumba ulimwengu leo. Wasomi wengi wa Kimagharibi pamoja na mufakirina wao wanao tishio la Uislamu la kuibuka tena kuwa taifa kuu duniani litakalo ondosha mfumo muovu wa kirasilimali. Kwa maana haya ndio huita misimamo mikali kama jaribio lao la kupambana na Uislamu. Kwenye mahojiano na shirika la Utangazaji la Uingereza BBC aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza Tony Blair alitamka wazi kuwa Uislamu unaolenga mapinduzi ndio tishio kubwa leo linalokabili dunia.

Kwa kupiga darubini vita dhidi ya ugaidi na kwa ujumla mipango yote ya kupambana na misimamo na itikadi kali tunapata kwamba michakato yote inalenga yafuatayo:-

**Kwanza,** kuubadilisha na kuufanya Uislamu kuwa ni Usekula; yaani Uislamu ujulikane kuwa hauna suluhisho kwa matatizo ya wanadamu hapa duniani. Kwa maana hii ni kutaka Uislamu ufundishwe kama Dini isiyokuwa na sheria zinazohusu maisha ya wanadamu badali yake kuwataka Waislamu wajifunge na Urasilimali na fikra zake za kihuria. Jambo hili linajenga athari mbaya sana kwa mabongo ya Waislamu kwani huwafanya watupilie mbali Dini yao na kukubali fikra matata za uhuru jumla. Ili kukabiliana na njama hizi Waislamu wawajibike kukataa mipango yote hiyo miovu na waingie katika mijadala na wasomi, mufakirina na watengeza sera katika kuwaonyesha taswira halisi ya Mfumo wa Kiislamu.

Umma wa Kiislamu lazima ufahamu kwamba kuishi Kiislamu kifikra na kivitendo ni amri kwao wao wala sio suala la kukhiyarishwa. Umma unapaswa aidha kufichua fikra za kihuni na mbovu za kisekula ambazo kiukweli kabisa ndio chanzo cha muozo wa kimaadili duniani. Na kwa kuwa kufeli kwa siasa ya kisekula ya Kidemokrasia jinsi inavyosababishia maafa na vurugu kunashuhudiwa wazi kote duniani…hili lafaa litie chachu kwa Waisamu kuleta mabadiliko msingi kwa ulimwengu mzima.

**Pili,** kuachana na ulinganizi wa kuwa Uislamu ni Dini iliyo na sheria na hukmu kamili ambazo hazitekelezeki kikamilifu ila kupitia serikali ya Khilafah. Kujitokeza kwa kundi la ISIS hata hivyo, na matendo yake ya kuuwa wasiokuwa Waislamu na Waislamu kumefanya kampeni kubwa ya kiulimwengu dhidi ya Khilafah kushika kasi na wote wanaolingania kusimamishwa kwa Khilafah wamepachikwa jina la wenye itikadi kali. Pasina shaka yoyote Wamagharibi wanatambua vyema kwamba Khilafah sio ndoto bali imekua ndio hitajio kubwa la Umma wa Kiislamu ambalo muda wake umefika. Kwa hivyo Wamagharibi wameshikwa na uendawazimu na wanafanya kila wawezalo kuzuia kusimamishwa tena Khilafah. Wao wanaiona Khilafah kama serikali kubwa yenye nguvu itakazozuia uchu na tamaa zao.

Kukabiliana na changamoto hii, Waislamu lazima kufahamu vyema suala la Khilafah na njia yake ya kuisimamisha. Lazima wafahamu kwamba Khilafah ni moja wapo ya hukmu za kisheria na wala sio maoni yatokayo kwa baadhi ya Waislamu. Khilafah ni hukmu ya Kiislamu ya kiutawala ambayo kupitia

*Endelea Uk..8*

kwayo Uislamu kama mfumo kamili huweza kutekelezwa kikamilifu.

Njia ya kuisimamisha serikali hiyo pia ni hukmu ya kisheria iliyochukuliwa kutoka kwa seera ya Mtume Muhammad (saw). Kwa kuiangalia seera hiyo ya Mtume (saw) akiwa Makka, Waislamu watakuta kwamba njia ya Mtume (saw) ya kusimamisha serikali hakuhusisha kabisa utumiaji wa mabavu au fujo bali ilihusisha mvutano wa kifikra na mpambano wa kisiasa. Jamii za kibinadamu haziwezi kubadilika kupita matumizi ya nguvu wala fujo bali ni kwa kupitia mivutano ya kifikra. Kinyume na Demokrasia ambayo watawala kama Bush na Blair waliieneza kwa Waislamu kupitia uvamizi wa kijeshi. Kwa mfano Iraq, vikosi vilivyoongozwa na Marekani viliuwa maelfu ya watu chini ya mwito wa kuikomboa Iraq kutoka kwa udikteta wa Saddam.

**Tatu,** Kufanya kazi ya kutia mpasuko katika amali ya Da'wah na amali ya kisiasa ya harakati na vyama vya Kiislamu. Makusudio yake ni kuwa kundi lolote la Kiislamu la kisiasa lisilojihusisha na njia ya mabavu katika kufikia malengo yake pia liitwe kundi lenye misimamo mikali. Hivyo basi, Wamagharibi hawaruhusu uwepo wa kundi linalofanya kazi ya kisiasa kwa kusema kwamba Dini haina mahusiano na masuala ya kisiasa hivyo da'wah lazima ifungike kwa masuala ya kiroho tu na masuala ya kibinafsi kama Ibadah, Akhlaq, Ndoa na Talaka. Ni kosa kubwa sana bali ni dhambi kuifunga Itikadi ya Kiislamu kiroho tu ionekana kama dini nyinginezo mfano wa Ukristo, Ubudha, na Uhindu. Kwa bahati mbaya baadhi ya vyama na makundi ya Waislamu yamebuniwa kwenye misingi hiyo hiyo ya kiroho; yaani yanawalingania watu kwa ibada tu za kiroho. Makundi haya ima kwa kujua au kutojua hulingania usekula na hatimaye kuishia tu kuhudumukia ajenda za kikoloni.

Ingawaje kulingania watu kwa ibada na kuwahimiza kushikamana na sunna ni amali inayopendekezwa kufanywa kwani kihakika pia ni sehemu ya da'wah lakini uhalisia ni kuwa da'awa hiyo haihusiani kabisa na kukabili tatizo linalowakumba Waislamu leo. Ukweli ni kuwa uhalisia wetu leo unatutaka kuutafakari kwanza kabla hatuja chukua hatua ya kutenda. Tukiangalia uhalisia wa Waislamu leo tunakuta kwamba Waislamu katika nchi yoyote ya Waislamu licha ya kubakia kwetu kuwa Waislamu bado tunaishi ndani ya -mujtama usiokuwa wa Kiislamu (Dar-ul Kufri). Huu ndio ukweli wetu ambao ni hali iliyoanza pindi ilipovunjwa Khilafah mwaka 1924. Kuondoka kwa Khilafah ndio kukasababisha hali hii mbaya tulionayo. Cha kutisha zaidi Sheria za Mwenyezi Mungu (swt) zimewachwa na kuchukuliwa mahala pake na kanuni za wanadamu!

Wazi kabisa suala nyeti linalowahusu Waislamu baada ya tukio la kuhuzunisha la kuvunjwa kwa Khilafah sio jengine ila kuutabikisha Uislamu katika nyanja za maisha yetu kibinafsi, kijamii kwa ujumla na ndani ya Serikali nayo ni kupitia tu kwa kusimamishwa kwa Khilafah na kuchaguliwa Khalifa wa Waislamu. Kwa kusimamishwa Khilafah nchi zetu zitabadilika kuwa Dar ul-Islam na jamii yetu kubadilika kuwa ni mujtama halisi wa Kiislamu, kuunganisha ardhi zetu kuwa chini ya mwavuli wa serikali ya Khilafah. Na hapo Uislamu uweze kubebwa kwa ulimwengu mzima kwa njia ya da'wah na Jihad. Suala hili ni suala la kufa na kupona kwani lahitajia Umma kujitolea mhanga.

Kwa hivyo da'wah lazima ijikite katika kuwalingania watu kuuchukua Uislamu wote kiaqeeda yake, ibada, akhlaq na miamala, mihimili ya serikali, uchumi, nidhamu ya kijamii, elimu na sera za nje na sheria zote za Mwenyezi Mungu. Hivyo kuufunga ulinganizi katika masuala tu ya kiibada hakuna mahusiano yoyote na kadhia hii nyeti kwa Waislamu na kwa hakika da'wah hiyo haitotufikisha kwa lengo kuu.

Kwa malengo hayo, mpango mzima huu wa Wamagharibi ni kuupinga Uislamu na utekelezwaji wake ndani ya Umma wa Kiislamu. Jaribio hili ni kuwatia chuki wasiokua Waislamu wawe na fikra mbaya dhidi ya Uislamu huku pia ukilenga kutia hofu Waislamu wasiweze kushikamana na sheria za Kiislamu kama zilivyomteremkia Mtume (saw). Kwa upande wa pili, ni kuwataka washikamane na maadili mabaya ya usekula. Hivyo Umma wa Kiislamu unapaswa kuamka na kuulingania Uislamu kwa njia safi na wazi ya kifikra na kisiasa pasina na kujihusisha na matendo ya kimabavu ili kuwapa wanadamu sura kamili ya Uislamu kuwa ni muongozo wa wanadamu wote.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Uharibifu Mkubwa dhidi ya Familia (Sehemu ya 1): Urasilimali Unamfedhehesha Mama

Neno uharibifu hivi sasa nimaarufu linajadiliwa katika muktadha wa uchumi wa kidijitali kwamba ni kukosa umakinifu kwa biashara duniani kwani njia za kibiashara za zamani zimepitwa na wakati. Lakini maana ya uharibifu katika makala haya ni hasa fujo na machafuko yanayo athiri mamilioni ya familia kutoka Magharibi kuelekea Mashariki na limekuwa janga la kibinadamu ambalo limesababishwa pakubwa na msukumo wa harakati za kuwawezesha wanawake. Katika hali yake ya usasa, ukombozi wa wanawake ukioanishwa na nidhamu ya kiuchumi ya kisekula, ambayo kumezaliwa zama mpya zenye uharibifu wa umama ambao hauathiri tu wanawake Waislamu bali pia unawanasa kina mama ndani ya nchi zisizokuwa za Waislamu hususan Magharibi na Asia-Pacific.

Sehemu ya kwanza ya makala hii itatathmini namna huu uharibifu unavyosababishwa na uhamiaji wa ukombozi wa wanawake unaochochewa na nidhamu ya kiuchumi ya kisekula katika kuwapatiliza kina mama, hivyo basi imekuwa na dori ya moja kwa moja katika kuwatelekeza mamilioni ya watoto na kuzidi kwa idadi ya talaka. Kisha katika sehemu ya pili, tutatathmini namna uhuru, moja ya sehemu ya misingi ya usekula urasilimali ulivyo sababisha kupungua kwa idadi ya familia na hata kupelekea kuhatarisha maendeleo.

**Uhamiaji wa ukombozi wa wanawake: Ukoloni mkubwa juu ya Umama**

Tangu kuzinduliwa kwake, urasilimali kiuhakika daima unawadharau wanawake na unawaangalia kama wafanyikazi duni au njia za uzalishaji. Kilele cha dori ya wanawake ipo tu katika kuwanasibisha na lugha ya kiuchumi – nako ni kuzalisha mada na faida katika biashara za kirasilimali. Maslahi maovu ya urasilimali katika siku zake za mwanzo yalikuwa yamefunikwa na fikra za ukombozi wa wanawake na pazia ya miito ya kuwawezesha wanawake ili ionekane tamu.

Lakini katika zama hizi za uharibifu, uso wa kweli wa Urasilimali unafichuka kwa kasi. Ulafi wake umewafanya kina mama kupatilizwa pakubwa hususan wale walioko katika eneo la Asia-Pacific kama soko la mwisho katika matumaini ya Urasilimali unaofariki. Eneo hili linakumbwa na uhamiaji wa ukombozi wa wanawake ambao umesababishwa na matarajio ya kirasilimali yasiyokwisha ya ukuaji wa uchumi. Matarajio haya yameangaziwa wazi katika hotuba ya Hillary Clinton katika Wanawake wa APEC na Jukwaa la Uchumi, 29 Juni 2012 ambapo alisema, "Wanawake sasa wanawakilisha asilimia 40 ya wafanyikazi duniani, asilimia 43 ya wafanyikazi wa kilimo duniani, na ni zaidi ya nusu ya wanafunzi wa vyuo vikuu duniani. Kwa hiyo inaingia akilini: Kwa kudhibiti uwezo wa kiuchumi kwa wanawake ni kwa kila nchi kama kuwacha pesa mezani. Haingii akilini hususan wakati ambapo tunajizatiti kujikuza ili kutoka katika janga la kiuchumi."

Matamshi ya Clinton yanafichua wazi dhamira ya kweli ya nchi za kirasilimali ambazo zinamoyo wa kuwatoa kafara wanawake kwa sababu wanawatizama kama wafanyikazi tu na injini ya ukuwaji wa uchumi. SIO kama kina mama wa kizazi kijacho na heshima inayostahiki kulindwa. Urasilimali kwa makusudi unawafedhehesha kina mama ni wafanyikazi tu, hata wakiwango cha chini. Kwa mujibu wa ripoti ya ILO 2013, wanawake milioni 43 wameajiriwa kama mayaya, wapishi, wasimamizi wa nyumba na vijakazi. Ilidhihirisha ongezeko kubwa la idadi ya milioni 19 ya wanawake walioajiriwa kama wafanyikazi wa nyumbani kwa zaidi ya takribani ya miaka 18 iliyopita. Umasikini na ukosefu wa ufanisi kwa mamilioni ya wanawake ndani ya nchi zao kumewalazimisha kuwacha nyumba zao na watoto wao ili kwenda kutafuta maisha. Wengi wa wafanyikazi wa nyumbani wanatoka katika nchi za ulimwengu wa tatu zikijumuisha ulimwengu wa Waislamu. Wengi wakitoka Asia Pacific (milioni 21.4), wakifuatiwa na Latin Amerika na kisha Caribbean ikiwa na milioni 19.6. Ni utekelezwaji wa urasilimali duniano na mpangilio wake wa kifedha wa riba na nidhamu yake ya masoko huru pamoja na misingi yake ya uhuru ambayo imesababisha utajiri kurundikana katika mikono ya wachache na natija yake ni kusababisha uhamiaji wa ukombozi wa wanawake kwa sura ya wafanyikazi wa nyumbani na kuwapelekea kunyanyaswa.

**Makumi ya Mamilioni ya Watoto wanawachwa nyuma**

Fikra ya sumu ya ukombozi wa wanawake kwa ushirikiano na ulafi wa urasilimali daima hautilii maanani athari yake juu ya watoto, familia na jamii kwa ujumla. Athari hii kubwa imetolewa ilani na Vannesa Tobin, naibu mkurugenzi wa New York wa Umoja wa Mataifa wa Mfuko wa Watoto (UNICEF) ambaye alisema kwamba tafiti kadhaa zimeonyesha kwamba gharama za kijamii zinazotokamana na uhamiaji wa wafanyikazi zinashinda zile za manufaa ya kiuchumi, huku mahusiano na mabadiliko ya kifamilia yakiathiriwa kwanza. Tobin alisema kwamba kuzidi kwa uhamiaji wa "ukombozi wa wanawake" umezidisha matatizo kwa kuwa inamaanisha "kubadilisha upya dori ya kiuchumi ya wanawake katika mujtama na ndani ya familia." (2008, Kongamano la Kimataifa Kuhusu Jinsia, Uhamiaji na Maendeleo)

Uharibifu wa umama, kwa kuongezea na kutikiswa kwa taasisi ya ndoa daima imezalisha uwepo wa kizazi kisichokuwa na msingi, chenye matatizo na kilichotelekezwa na ikiwa ni natija ya taifa ambalo linawaajiri kina mama kama injini za ukuwaji wa uchumi. Tume ya Indonesia ya Ulinzi wa Watoto (2016) ilichapisha taarifa kuhusu mamilioni ya watoto wachanga waliotelekezwaa na mama zao ili kwenda kufanya kazi ng'ambo. Wapo watoto wa Indonesia milioni 11.2 waliokosa malezi ya wazazi na mapenzi kutoka kwa mama zao, ilhali taarifa za UNICEF (2008) zinaashiria kwamba takribani watoto milioni 6 ndani ya Filipino wametelekezwa kwa kuwa mama zao wamekuwa wafanyikazi wahamiaji. Watoto waliotelekezwa pia wanakabiliwa na matatizo wanapo hamia ng'ambo na mama zao ambao ni wafanyikazi wahamiaji. Ndani ya Sabah – Malaysia – inakadiriwa kwamba kulikuwepo na takribani watoto elfu 50 kutoka kwa wafanyikazi wahamiaji wa Indonesia ambao hawapati haki nzuri za elimu. Ndani ya Hong Kong, pia nako kunalo suala la "watoto ambao hawakusajiliwa" waliozaliwa kutokana na mamia ya maelfu ya wafanyikazi wahamiaji wa Indonesia na Filipino.

Uhamiaji wa kiuchumi umewatenganisha mamilioni ya watoto kutoka kwa mama zao nalo pia linatokea ndani ya Uchina. Kwa mujibu wa Muungano wa Wanawake Wote wa Uchina

*Endelea Uk..10*

na UNICEF (2016) wapo watoto milioni 61 ndani ya Uchina waliochini ya umri wa miaka 17 ambao wamewachwa katika maeneo ya vijijini huku mzazi mmoja au wote wakihama kutafuta kazi. Zaidi ya watoto wanaume na wasichana milioni 30 wengine wakiwa na umri wa miaka minne wanaishi katika shule za mabweni za serikali katika vijiji mbali na wazazi wao na mara nyingi mbali na nyanya/babu zao au walinzi wao. Watoto hawa waliotelekezwa ndani ya Uchina wanakabiliwa na matatizo mengi kama usafirishaji wa watoto, vurugu za kijinsia, kujiua, uhalifu na maradhi mengine ya kimujtama kama yalivyofanyiwa utafiti na Li Yifei (2015), Profesa kutoka Chuo cha Beijing Normal. Hii ndiyo athari ya uharibifu wa umama ndani ya mujtama wa kisekula ambao uko mbali na nuru na muongozo wa Uislamu. Kumbuka Mwenyezi Mungu (swt) asema”

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى

“Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.” (Ta Ha, 20:124)

Kuwawezesha wanawake kukubwa ndani ya Uislamu ni kuwajenga katika dori yao kama walinzi wa mujtama na walimu wa kizazi kijacho, SIO kama kikosi cha wafanyikazi. Katika Kielelezo cha Katiba cha Hizb ut Tahrir (Muqaddimah Dustur), katika kipengee kinachohusiana na Nidhamu ya Kijamii ya Uislamu (“Nizam al-ijtima’i”), kinasema, “jukumu msingi la mwanamke katika Uislamu ni kama mama kwa watoto wake na msimamizi wa nyumba ya mumewe. Mwanamke ni heshima inayostahiki kulindwa.”

Mfano wa Uislamu uko kinyume na Urasilimali. Uislamu haswa unahifadhi mahusiano mazuri baina ya jukumu la umama la wanawake na ubora wa kizazi kijacho kwa kuhakikisha kuwa maumbile ya umama yanabakia kwa ukamilifu ndani ya jamii na kuhakikisha kudumu kuzaliwa kwa kizazi bora kupitia uungwaji mkono na nidhamu za elimu, kijamii na kiuchumi za mfumo wa Kiislamu, illhali wakati huo huo zikiwadhamini wanawake kupata haki za kielimu, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Uislamu unaamrisha kwamba wanawake lazima wadhaminiwe matumizi kutoka kwa jamaa zao wanaume, na lau watakuwa hawana jamaa yeyote mwanamume, basi dola itahakikisha kuwa inawakidhia mahitaji yao ya kifedha.

Mjadala kuhusiana na kuendelea kwa athari za uharibifu juu ya umama katika familia na mtizamo wa Uislamu juu ya ujenzi wa familia madhubuti utatathminiwa katika sehemu ya pili ya makala hii.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Fika Komara**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Uharibifu Mkubwa dhidi ya Familia (Sehemu ya 2): Uhuru Unapunguza Idadi ya Familia

Maana ya uharibifu katika makala hii ni fujo na machafuko yanayo athiri mamilioni ya familia kutoka Magharibi kuelekea Mashariki na limekuwa janga la kibinadamu ambalo limesababishwa pakubwa na msukumo wa harakati za kuwawezesha wanawake. Katika hali yake ya usasa, ukombozi wa wanawake ukioanishwa na nidhamu ya kiuchumi ya kisekula, ambayo kumezaliwa zama mpya zenye uharibifu wa umama. Sehemu ya kwanza ya makala hii ili tathmini moja ya sababu ya uharibifu huu nao ni uhamiaji wa ukombozi wa wanawake unaosukumwa na nidhamu ya kiuchumi ya kisekula inayopatiliza kina mama, hivyo basi imekuwa na dori ya moja kwa moja katika kuwatelekeza mamilioni ya watoto.

Hivi sasa katika sehemu ya pili tutatathmini namna uhuru, ukiwa ni moja ya misingi muhimu ya usekula urasilimali namna ulivyo sababisha idadi ya familia kupungua na hata kupelekea katika kuhatarisha mujtama kutokana na sera ya "wanawake na uchumi".

**"Kifo cha Familia" ndani ya Ulimwengu wa Kisekula wa Viwanda**

'Kifo cha familia' kinaangaziwa na janga la ukosefu wa uzazi ndani ya Japan. Linasababisha madhila ya kiuchumi na kijamii ambayo hayajawahi kuonekana kama ilivyoelezewa na Mary Brinto, mwanasosholojia wa Harvard kwa Business Insider mwaka jana. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nalo pia lilionya nchi nyingine za Asia ziwe macho zisifuate mkondo wa Japan wa "kuwa mtu mzima kabla kuwa tajiri." Mnamo 2016 ripoti ya UBS ilionyesha kubadilika kwa mitazamo kuelekea ufanyajikazi na dori za kijinsia kuwa kutapelekea mataifa ya viwanda ikijumuisha Amerika kupata uzito sawa na wa kiuchumi. Hofu ya jamii za kiuchumi nyingi ni mwenendo wa idadi ya watu unaodhihirika duniani utapelekea mataifa mengi yenye uchumi mkubwa kutaabika kama inavyotaabika Japan. Kwa maana nyingine watu wanawasiwasi kwamba uchumi wa dunia utabadilika kuwa kama wa Wajapani.

Sera ya kirasilimali ya "wanawake na uchumi" ndani ya Japan, ambayo ni mazao ya uchumi wa uhuru unawalazimisha wanawake kufanyakazi lakini kila wanawake wengi walipokuwa wafanyikazi nao uzazi ukaanza kushuka. Leo, uzazi wa Japan uko kwa kiwango cha 1.41. Natija yake ni kwamba idadi ya watu inapungua ilhali unyama wa kufanyakazi masaa mengi unaendelea. Kwa zaidi ya miongo miwili, hadithi kuhusiana na wanandoa wachanga Wajapani walikuwa wakipigana ili kufaulisha mahusiano yao ndani ya tamaduni ya ufanyajikazi unaowatarajia wanaume kuwa ndio wachumaji na wanawake ndio wasimamizi wa nyumba wakiwasilishwa kuwa ni vita ambavyo haviwezi kufaulu. Bali wanandoa wengi wanalazimishwa kutizama muda wao ukipotea na wakisalimisha kila kitu kutoka siku ya usiku wa kukutana ili kuanza familia. Wakati huo huo, wanawake wengi wanatizama kuajiriwa kuwa ni kuwapa cheo cha juu kuliko umama, na kuwapelekea wengi kupoteza nishati ya kuwa wake na kupata watoto wengi.

Janga la uzazi pia limeikumba Korea Kusini. Utafiti wa Baraza la Huduma za Utafiti la Kitaifa (NARS) ndani ya Seoul mnamo Agosti 2015 lilipendekeza kuwa kuna uwezekano mkubwa wa Korea Kusini kupotea kutokana na kupungua kwa idadi ya kuzaana na kuwa chini ya 1.19 kwa kila mwanamke mnamo 2013. Ili kujibu hilo, jarida la The Diplomat lilielezea kuwepo kwa tishio kubwa la idadi ya watu kwa maana ya Kupotea kutalikumba eneo hilo na sio tu Korea Kusini na Japani. Taiwan na Singapore nazo pia zinapambana kugharamikia kifedha idadi kubwa ya watu wazee kutokana na kupungua kwa watu jumla. Ni kinaya na kituko kwamba nchi ambazo zinatajwa kuwa ndio "Maajabu ya Asia Mashariki" kutokana na kufaulu kwao katika kubadilisha na kuwa eneo lenye uchumi mkubwa sasa hivi yanakodolea hatari ya vizazi vyao kuangamia kama taifa.

Takribani sawia na majirani zake ndivyo hali ilivyo ndani ya Uchina. Gazeti la The People's Daily liliripoti mnamo Disemba 2016 kwamba Uchina ya viwanda nayo pia kwa haraka inakaribia kuwa nchi ya makapera na wari kwa kuwa idadi ya watu wake ambao hawajaoana inakaribia milioni 200. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Tencent mnamo 2016, asilimia 36.8 ya wanawake Wachina ambao hawajaolewa wanaamini kuwa ndoa sio jambo la msingi ukitaka kuishi maisha ya furaha. Wafuatiliaji wa idadi za watu wanaamini kwamba uhuru wa wanawake Wachina wa sasa ni moja ya sababu ya kuwepo kwa idadi ya watu ambao hawaoani. Uchina – ndio nchi yenye watu wengi duniani – nayo pia itapungua watu kama inavyowafuata wakuu wake Wamagharibi kama ilivyo pia ndani ya Mashariki, Japan na Korea Kusini. Idadi kubwa ya wanawake ambao hawajaolewa nayo pia itafuatiwa na kupungua kwa idadi ya kuzaana ambayo hatimaye itapelekea idadi ndogo. Haya yanatokea katika kila nchi ya kirasilimali ambayo imepanuka kiuchumi. Wanawake wanapoweka kipaombele ni kufaulu kimadaniya na hawazingatii kujenga familia, hawakiamini kiapo cha ndoa na hata kuwatizama watoto kuwa ni mzigo wa kiuchumi basi hili kiukweli ni dalili ya mwanzo ya kufariki kwa taifa ambalo linaendelea kuzeeka likisubiri kifo chake. Ni taifa ambalo haliwezi tena kudhibiti madhara makubwa katika maisha yake ya kijamii ndani ya mujtama wake – italipa gharama kubwa kutokana na ukuwaji wa uchumi wake iliyokuwa inautafuta kwa gharama yoyote.

Nchi za Kimagharibi ndizo hasa zilizokuwa zinakuza majanga haya ya kijamii kabla ya nchi za Mashariki ya Asia na kutoka kwao ndipo tunapojifunza kwamba "kifo cha familia" hakisukumwi tu na uhuru wa kiuchumi pamoja na 'wanawake na uchumi'; bali pia inajumuisha uhuru wa jamii pamoja na misingi ya ubinafsi ambayo imesababisha majanga makubwa ya kiafya. Hali hizi kimsingi zinaangamiza maisha ya familia na zimepelekea kuwepo na nchi za ukame wa watu katika nchi nyingi za Ulaya na Amerika. Mnamo Januari 2018, Uingereza (UK) ilimteua waziri wa upweke ili kupambana na kile ambacho Waziri Mkuu Theresa May alikitaja "uhalisia wa majonzi ya maisha ya kisasa" kwa watu wengi kwa maana zaidi ya watu milioni 9 daima huwa wanajihisi kuwa wapweke na takribani wazee 200,000 nchini hawajawahi kuwa na mazungumzo na rafiki au jamaa zaidi ya mwezi. Lakini watu wa UK hawako peke yao katika upweke. Ndani ya Amerika (US), kama makala ilivyoandikwa ndani ya Harvard Business Review, "Upweke ni janga la kiafya linaloendelea kuongezeka. Tunaishi ndani ya zama ambazo teknolojia imetuunganisha zaidi katika historia ya wanadamu, lakini bado upweke umezidi maradufu tangu miaka ya 1980, leo zaidi ya asilimia 40 ya watu wazima ndani ya Amerika wanaripotiwa kuhisi upweke, na utafiti

*Endelea Uk..12*

unapendekeza kwamba idadi kamili inawezekana kuwa juu zaidi.”

**Uislamu Unatoa Suluhisho la Kudumu kwa Familia**

Mawimbi makali ya uharibifu ambao yanaukumba muundo wa familia ndani ya nchi za kisekula za viwanda yamepelekea “kifo cha familia”, hivi sasa yanaendelea kuhisika ndani ya ardhi za Waislamu. Ndani ya Malaysia, kwa mfano matarajio ya kutafuta maendeleo na cheo kama ilivyo katika nchi zilizoendelea zimeipelekea Malaysia kukodolea hali ya “Maradhi ya Thaqafa ya Chicago” ambapo ni taifa ambamo watu wanapata mapato makubwa lakini linafuatiwa na kusambaratika kimaadili. Profesa kutoka katika Taasisi ya Kimataifa ya Watu na Fikra ya Kiislamu (ISTAC), Mohd. Kamal Hassan aliionya serikali ya Malaysia ISIkuze dalili sawa na za Magharibi. Alisema, “Pia inatokea ndani ya Malaysia na itakuwa mbaya zaidi lau haitodhibitiwa kwa sababu misingi ya maadili na kujiheshimu binafsi kukochini, hili ni kubwa kupitia uhalifu kama vile kupora mpaka kifo, kuua na kubaka.” Hakika huu ndio wasifu wa nchi za kisekula za viwanda hivi leo, ambapo maendeleo makubwa yanafuatiwa na majanga ya kijamii, kuporomoka kwa taasisi ya familia, kusambaa kwa uhalifu, vurugu dhidi ya wanawake na watoto na idadi kubwa ya kujitoa uhai kwa kuongezea na kushuka kwa idadi ya kuzaana ambayo kwa kiasi kikubwa ni kutokana na kuhusishwa kwa wanawake katika ufanyajikazi. Inadhihirisha ufinyu wa mtazamo wa kimfumo wa dola za kisekula za kirasilimali kwa kupatiliza madaniya na maslahi ya kiuchumi na kupuuza furaha ya familia na mujtama kwa ujumla.

Hivyo basi ni suala nyeti kwa Waislamu kurudi katika mafundisho ya Kiislamu na kujihusisha pasina kusita katika kampeni ya kuitekeleza nidhamu ya kisiasa tukufu ya Kiislamu katika kuhifadhi kizazi cha binadamu na kudumisha uzuri wa ustaarabu wa Kiislamu. Kumbuka Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.” [An-Nisa’: 1]

Mafundisho ya Kiislamu yanaweza kuwa ni njia yenye nguvu katika kuhifadhika katika zama hizi za uharibifu. Msingi muhimu wa mafundisho ya Kiislamu kattu hayawezi kupitwa na wakati na daima yatakuwa sambamba na familia ya zama hizi na hivyo basi lazima tujifunge nayo kikamilifu: Miongoni mwayo ni:

1. Uislamu unashaajiisha ndoa na kuzisifu taasisi za ndoa kuwa ndio njia pekee ya kuhifadhi kizazi.
2. Uislamu pia inazo hukmu za familia ambazo zinapangilia majukumu ya waume na wake ili kuweka maisha ya amani ya familia makini pamoja na kuasisi utulivu baina ya wanandoa.
3. Uislamu unasisitiza kuhusu ubora wa jukumu la umama kwa wanawake.
4. Lengo la ndoa katika Uislamu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu (swt) kwa maana ni kuhifadhi kizazi na kupatikane amani (utulivu/ sakinah, mapenzi/ mawaddah na kuhurumiana/ rahmah), sio tu kukidhi haja ya kijinsia au kwa ajili ya kupata cheo katika mujtama. Hivyo basi, Uislamu umesisitiza msingi na umuhimu wa kuwepo na akili tambuzi katika kukifunza kizazi kilichopo na kijacho.
5. Uislamu umeweka msingi wa itikadi na kuamini (tawakul) katika Rizq kwa Waislamu ili isiweze kuyumbisha mpangilio wa majukumu ndani ya familia, kwa maana kuwa wanaume ndio wachumaji wa familia.
6. Uislamu unayo nidhamu ya kiuchumi ambayo inabuni uchumi mzuri, unaozalisha na ulio na uwezo wa kuondosha ukosefu wa ajira mkubwa, kuhakikisha kunapatikana mahitaji msingi ya raia na wakati huo huo unawaruhusu watu binafsi kuweza kupata mahitaji ya ziada. Msingi wa sera zake umeelekezwa katika kusambaza utajiri ili kudhamini mahitaji mzingi ya raia wote, kuzuia ukandamizaji wa kiuchumi na unyanyasaji wa wanawake. Napia itawawezesha wanaume kutimiza majukumu yao ya kukidhi mahitaji ya kifedha kwa familia zao ilhali wakati huo huo dola imewajibishwa kuwapa wanawake ambao hawana jamaa wakiume msaada.
7. Uislamu umewawajibisha watawala Waislamu kuungana chini ya kivuli cha Khilafah ya Kiislamu kwani ndio kivuli cha kweli cha Waislamu ambacho kitailinda familia, heshima ya kina mama na kukitukuza kizazi cha Waislamu na kuwapa hadhi. Wakati huo huo Khilafah itailinda familia kutokana na machafuko ya ulafi wa Urasilimali na mizozo ya kijamii inayosababishwa na uhuru.

Hivyo basi, Khilafah itaweza kujenga familia madhubuti na kuangamiza vigezo vyote ambavyo vinaiharibu kama ilivyodhihirishwa katika matamshi ya Uthman (ra): “Hakika Mwenyezi Mungu anampa madaraka mtawala ili kuondosha kile ambacho hakiwezi kuondoshwa na Qu’ran.” Wallahu a’alam.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Fika Komara**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# SWALI/JAWABU:
# Ni Upi Uhalisia wa Mzozo wa Kimataifa na Ushawishi wake ndani ya Algeria?




**Swali:**

Katika nchi ambayo watu wake wameubeba Uislamu, nchi ya mashahidi milioni moja kwa kupigana jihad dhidi ya uvamizi wa Ufaransa uliokuwepo kwa miaka 132, ndani ya nchi maandamano yaliyoungwa mkono na wengi yalianza, yakivunja vizuizi vya hofu kwa madhalimu wa Algeria tangu 22/2/2019 mpaka wa leo, lakini hawalinganii Uislamu! Ni zipi sababu za hilo? Ni upi uhalisia wa mzozo wa kimataifa na ushawishi wake ndani ya Algeria? Je una dori katika yale yanayotokea? Na kutarajiwe nini hususan kuhusiana na uchaguzi?

**Jawabu:**

Ili kupata jibu kwa maswali hayo, tunatathmini yafuatayo:

**Kwanza: Sababu ya kutolingania Uislamu katika harakati:**

1- Naam, Algeria ni nchi ya Uislamu sahihi na hilo lilithibitishwa pale ambapo dola ilipotoa nafasi ya uchaguzi huru na wa haki mwanzoni mwa miaka ya 1990. Natija yake ilikuwa ni kutokana na ulinganizi mkubwa wa kutaka kuhukumiwa na Sheria za Mwenyezi Mungu ambao ulibebwa na mamilioni katika barabara za Algeria. Ulaya ilikasirika na Ufaransa kutishia kuingilia kati kijeshi. Ulaya na Ufaransa iliwasukuma watawala wa Algeria mwanzoni mwa 1992 kupinga matokeo ya uchaguzi wa 1991, kisha jeshi likaingilia kati na kutangaza udhibiti wake juu ya nchi. Uungwaji mkono mkubwa kwa watawala ulitoka kwa miji ya kiza, “Paris,” ambayo kiurongo inaitwa miji ya nuru. Ujasusi wa Ufaransa kwa ushirikiano na taasisi za usalama za eneo zilichochea cheche za mauaji ya kidhalimu ambayo yalianzisha zama za mauaji ya miaka 1990 ambayo yaliua mamia ya maelfu ya Waislamu ndani ya Algeria. Kisha pasina aibu au fedheha, utawala wa Algeria na nyuma yake Ufaransa na Uingereza ikayanasibisha mauaji hayo na Waislamu wanaolingania Shari’ah ya Kiislamu. Janga hilo lilienea na utawala ukanasibisha kila tone la damu na mauaji hayo na Waislamu wanaolingania Shari’ah ya Kiislamu. Kipindi hicho kilichukua takribani miaka kumi na kuitwa “Muongo Mweusi” na utawala ulianza kueneza hofu katika akili za watu kutolingania Uislamu na kwamba yeyote anayelingania Uislamu uwe ndio unaohukumu anataka kurudisha miongo mieusi! Vyombo vya habari vya Kifaransa vililingania mwito huo wa kuogofya na

*Endelea Uk..14*

hofu ya Uislamu ikawateka wanasiasa wengi ndani ya Paris. Uoga wa Ufaransa na Uingereza na kutekwa na harakati za Algeria lau zingelingania Uislamu zimehama mara moja kwa utawala wa Algeria: "Pande husika zilizo karibu na kikundi kilicho na maamuzi ndani ya nchi kimepigia debe kwamba Waislamu wanaolingania Shari'ah ya Kiislamu 'watakwenda kinyume na masekula na kuwa na mpango wa dola ya Kiislamu ambayo itajengwa juu ya magofu ya masekula na labda hata miili yao ikihitajika" (The Independent 21/3/2019). Hivyo basi, utawala unawapa onyo watu mara moja kuhusu "sanamu la Uislamu wa siasa kali" ambao uko tayari kumwaga damu! Licha ya kwamba ni utawala ndio unaowafuatilia Waislamu na kumwaga damu. "Vikosi vya usalama vya Algeria vilimshambulia muasi maarufu na mmoja wa waanzilishi wa Islamic Salvation Front, Ali Belhadj na kumburuza katika barabara" (Arabic 21, 23/2/2019) katika siku ya pili ya kuanza kwa maandamano ya Algeria…!

2- Hili ni pamoja na vita vya Amerika dhidi ya Uislamu ambavyo vimechukua kichwa kipana cha "Ugaidi wa Kiislamu" ambapo mukhlisina katika ulimwengu wa Kiislamu na harakati, miungano na watu maarufu wamelengwa na kutengwa kwa ugaidi na kuzifanya alama za Kiislamu ni uhalifu kama vile mabango na wale wanaojifunga na dalili za Kiislamu kuwa ni wenye misimamo mikali na magaidi n.k. Yote haya yanaweka kivuli juu ya ulinganizi wa harakati maarufu ndani ya Algeria.

3- Moja ya sababu ya zilizopelekea kutochipuza kwa madai ya Kiislamu katika harakati za Algeria ni yale yaliyoganda katika akili za watu kuhusu baadhi ya harakati zilizo na sifa za Uislamu ambazo zinaitwa "poa". Wameziona baadhi ya wakati zinajiita harakati za upinzani na mara nyingine zikishiriki katika serikali na kufurahia vyeo vya uwaziri na ubunge. Kushiriki kwao huku kuliwaathiri watu wengi na hususan wale ambao walikuwa wanaziamini harakati hizi kuwa zinafanyakazi ya Uislamu na kisha kuziona zinafanya kazi na utawala. Pasina kutaja hukmu za Kishari'ah ambazo hawakujifunga nazo za kuharamishwa kwa sheria zilizotungwa na mwanadamu ndani ya mabunge na kuharamishwa kwa kushiriki katika tawala ambazo hazitokamani na Uislamu kwa sura yoyote ile. Hili limepelekea kwa kundi kubwa la Waalgeria kutotaja Uislamu ndani ya harakati hizo.

4- Mwisho kabisa, mzozo wa kimataifa ndani ya Algeria ili kutia ushawishi na majaribio ya kukata tamaa ya Wamagharibi hususan Ufaransa ili kueneza thaqafa ya kisekula na kuangazia uongozi ambao ni wafuasi wao katika harakati ambazo kwa uhakika ni za kisekula na kufaulisha hilo kupitia ushawishi wao wa kisiasa ndani ya Algeria. Tukizingatia kwamba pande husika katika mzozo wa kimataifa ndani ya Algeria unakubaliana kwa ukamilifu kuhusu kuangamiza utambulisho wa Kiislamu ndani ya Algeria na kuangazia sifa za kisekula za dola.

**Hizo ni baadhi ya sababu za kina ambazo zimepelekea kuchipuza kwa sifa za usekula katika harakati maarufu ndani ya Algeria; ambazo nyuma yake ni uhadaifu, upotoshaji na chuki za kisiasa za Wamagharibi na vibaraka wao. Na lau inadhaniwa watafaulu katika kuzuia kuchipuza kwa harakati ya Kiislamu, Uislamu umemakinika katika moyo wa Algeria kwa mashahidi milioni moja na kuchipuza kwake hakutocheleweshwa, na kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na kesho inakaribia,**

{إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً}

**"Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake." [At-Talaq: 3]."**

**Pili: Ama kuhusu mzozo wa kimataifa ndani ya Algeria:**

**1. Kwa Uingereza na Ufaransa:**

a- Tangu mapinduzi ya Boumediene mnamo 1965, ushawishi wa Uingereza uko juu ndani ya Algeria huku Ufaransa nayo ikiwa na baadhi ya nguvu. Lakini baada ya kufutwa kazi kibaraka wa Kifaransa Khaled Nizar kutoka katika Wizara ya Ulinzi mnamo 1993, ushawishi wa Ufaransa ulidhoofika polepole ndani ya jeshi mpaka ukafikia hatua ya kutegemea "thaqafa ya kijeshi" badala ya utiifu wa kisiasa. Bouteflika anajulikana kwa utiifu wake kwa Uingereza katika kipindi cha utawala wake tangu 1999 na amekuwa akitibu kujitanua kwa Ufaransa polepole pasina kuleta gumzo.  Suala la kusitisha ushawishi wa Ufaransa kutoka katika muundo wa dola ulikaribia kuwa mashindano ya riadha; kwani hakukuonekana ishara za kutokwa na jasho kutoka pande husika katika suala la ushawishi ambalo lilichukuwa sura ya mashindano. Lakini Bouteflika alipomfuta mkurugenzi wa Huduma ya Kijasusi, Mohammad Median anayejulikana kama Jenerali Tawfeeq mnamo 13/9/2015 lilikuwa ni pigo chungu kwa ushawishi wa Ufaransa ndani ya Algeria ambayo ilikuwa imefurushwa katika jeshi na kuendelea kutegemea ujasusi kama sehemu pekee ya nusu ya usalama kama ushawishi wa Ufaransa ndani ya Algeria. Pigo hilo chungu liliwasha moto chini ya majivu ya utulivu wa mahusiano baina ya washawishi wawili wa Algeria.

b- Kumekuwepo na hali mbili zilizopelekea ushindani baina ya ushawishi wa Uingereza na Ufaransa ndani ya Algeria kutoka kuwa ni wa ushindani wa kiriadha na hivyo mzozo baina yao ulikaribia kuwa "wakusokotana mikono" licha ya kwamba haikupelekea "kuvunjika kwa mfupa". Hali mbili hizi ambazo zimeyafanya mashindano baina ya nchi mbili kuwa moto ni:

Ya kwanza: kura ya maoni ya Uingereza kutoka Ulaya mnamo 2016 imepanua mzozo baina ya Uingereza na Ufaransa na hili lilidhihirishwa na ukazanishaji wa Ufaransa, Umoja wa Ulaya (EU) katika mazungumzo yake na Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May ambayo yalidhihirishwa katika mipango ya Waziri Mkuu mpya, Johnson ya kuondoka EU pasina makubaliano na haya ni madhara makubwa kwa Ufaransa. Kutokubaliana huko pia kulichipuza kuhusiana na suala la Amerika kusababisha janga na Iran baada ya kujitoa kutoka katika mpango wa nuklia. Ilhali Ufaransa ilikuwa imechukua mtazamo tofauti na Amerika nayo Uingereza ilikuwa inauunga mkono na tofauti zao ziliendelea kupanuka. Tofauti hizi mpya baina ya Uingereza na Ufaransa zinadhihirishwa na misimamo yao katika maeneo mengine kama Algeria.

Ya pili: kuanza kwa maandamano ndani ya Algeria mnamo 22/2/2019. Ufaransa iliona kwamba kukosekana kwa umakinifu ndani ya Algeria na kusukwasukwa kwa nguzo za ushawishi wa Uingereza ndani ya Algeria kuwa ni fursa ya kuurudisha ushawishi wake mkubwa ndani ya Algeria; kwa hiyo kuchipuza kwa harakati maarufu kumeufichua moto uliofichika wa Ufaransa tangu 2015!

c- Natija yake ni hali ya mashindano baina yao ambayo yamevuka na kuwa katika ngazi ya "kusokotana mikono". Huduma za usalama zimefichua mipango sawia ya mapinduzi ya kijeshi ili kumuondosha Qaid Saleh [Gaid Salah] kutokuwa mkuu wa majeshi kwa hiyo vikosi vya usalama viliwashika

***Endelea Uk..15***

wanaume wenye nguvu na hatari wa Ufaransa kama Mohamed Median (Jenerali Tawfiq) na Bashir Tartak wakurugenzi wa zamani wa huduma za ujasusi ambao walishikwa mnamo 5/5/2019. Kisha kushikwa kwa kiongozi wa Chama cha Labour Louisa Hanoune, mnamo Mei 5, 2019 na kuongezea na Said Bouteflika ambaye anaonekana kuwa wanaume wa Ufaransa ndani ya Algeria wamemvuta upande wao hususan baada ya kujiuzulu kwa kakake, Rais Bouteflika na walishtakiwa; "mahakama ya Kijeshi ya Algeria ndani ya Blida iliwahukumu washtakiwa wanne kwa shutuma za kupanga njama dhidi ya jeshi na mamlaka ya serikali kwa kifungo cha miaka 15 gerezani. Hukumu hizo zilizotolewa mbele ya Said Bouteflika, Louisa Hanoune kiongozi wa Chama cha Labour na Luteni Jenerali mstaafu Mohamed Medine. Mahakama ya kijeshi ndani ya Blida pia ilimuhukumu pasina kuwepo mahakamani Waziri wa Ulinzi wa zamani Khaled Nizar kifungo cha miaka 20 gerezani" (Sky News Arabic 25/9/2019). Ufaransa imepinga dhidi ya uongozi wa kijeshi ndani ya Algeria kwa sababu ya kushikwa huko. Kwa mujibu wa Gazeti la Uingereza la Independent mnamo 18/5/2019, wakati aliposhikwa Louisa Hanoune, Wafaransa 1000 wakijumuisha Waziri Mkuu wa zamani Jean-Marc Ayrault walitia saini mpango wa kumtaka awachiliwe. Gazeti liliongeza "naibu wa chama cha republican katika bunge la Ufaransa, Jean LaSalle alihofia athari ya matukio juu ya maslahi ya nchi yake" na kusema "Kunyanyuka kwa kizazi kipya cha maafisa na majenerali katika jeshi la Algeria lililo na muundo na mpangilio wa kitaifa unatishia maslahi ya Ufaransa ndani ya Algeria hususan katika mitizamo ya kithaqafa, kiuchumi na kisiasa." Hii ni ishara ya kuudhika kwa Ufaransa inayomaanisha kuwa mzozo huu unachuku mkondo wa joto licha ya hivyo Uingereza bado iko juu ndani ya utawala na ikiungwa mkono na mkuu wa majeshi.

**2 – Majaribio ya Amerika kujipenyeza ndani ya uga wa Algeria:**

Vyombo vya habari vya Amerika vimejaribu kuwapigia debe baadhi ya watu waliochipuza katika harakati maarufu kama vile Karim Tabbou, katibu wa zamani wa Socialist Forces Front. Chaneli ya Alhurra, American TV ilimzungumzia mnamo 12/9/2019 kama ("sura maarufu katika harakati zenye umaarufu" na kuzipigia debe video za Karim Tabbou "akiongoza maandamano ndani ya mji wa Algeria kama sehemu ya harakati zenye umaarufu" na kupigia debe "upinzani wa kweli dhidi ya uongozi, sio kama vyama vyengine"). Hili labda linaashiria kuwepo kwa mawasiliano ya Amerika na wanaharakati kama hao na wengine ndani ya harakati maarufu ndani ya Algeria. Huduma za usalama za Algeria zimemshika mwanaharakai huyu na wengine na kuwashitaki kwa "kudhoofisha hamasa ya jeshi." Kwa kuchukulia uwepo wa mawasiliano ya Amerika na ishara za harakati maarufu ndani ya Algeria, na hili linatarajiwa kwa hiyo watu aina hiyo bado hawajafikia uwezo wa kushawishi maisha ya kisiasa ndani ya Algeria kwa malengo ya Amerika na kwamba haijaweza kujipenyeza katika ushawishi wa kijeshi na taasisi za kiserikali kwa sasa.

**Katika yote haya, uga wa Algeria unakaribia kuwa hauna mzozo wa Ulaya na Amerika, bali ni mzozo baina ya Uingereza na Ufaransa ukikaribia jaribio la Uingereza na nidhamu yake ya kijeshi kuikata mbawa Ufaransa ndani ya uga huo. Majaribio ya Amerika hayakufaulu katika kujipenyeza katika dori ya Ulaya ndani ya Algeria licha ya kwamba kundi linalotawala ndani ya Algeria linahofia kuendelea kwa mzozo huo – harakati maarufu – inaweza kuiwezesha Amerika kufaulu ambako imekuwa inakutafuta kwa miaka, lakini kwa Ufaransa inaweza kutumia muda huo mrefu wa harakati ili kumakinisha wafuasi wake na kuwapa nafasi wao.**

**Tatu, ama kuhusu yanayotarajiwa kutokamana na uchaguzi, yanaweza kufahamika kama ifuatavyo:**

1- Uingereza na wale walioko madarakani na uongozi wa jeshi wameweza kuwatenga wanaume wa Ufaransa pakubwa kutoka katika muundo wa serikali, kwa hiyo nidhamu hii inaharakisha uchaguzi ili isiweze kubadilisha hali zilizopo hususan harakati zinazoendelea, Qaid Saleh alisema: "kabla ya sasa tulikuwa tunazungumza kuhusu umuhimu wa kuharakisha uchaguzi wa urais. Leo, tunauhakika kwamba uchaguzi huu utafanyika ndani ya muda uliotengewa." (Independent 14/9/2019) pamoja na ombi lake la kuwepo kwa msimamo wa wazi kama (kutangaza kwamba muda uliopo sasa unahitaji msimamo wa wazi "Hakuna nafasi ya kushika bakora kuanzia katikati… Ima uwe na Algeria au maadui wake" (The Independent 14/9/2019). Hii ni ishara kwamba mrengo wa nidhamu ya utawala unaoegemea Uingereza unaharakisha uchaguzi ili kulisuluhisha leo kwa sababu mambo yanaonekana kuwaegemea wao. Ufaransa na vikosi vinavyoiunga mkono wanapinga kutekelezwa kwa uchaguzi huo au wanapendekeza kuuhairisha mpaka pale hali itakapokuwa upande wao lakini hawatoi kauli mbele ya umma kuhusu hilo bali wanasema kidiplomasia kwamba uamuzi upo katika watu wa Algeria kuhusiana na masuala ya nchi yao!

2- Nidhamu ya serikali inajaribu kuwasukuma wagombea kutoka katika wafuasi wake ili kugombania uchaguzi wa urais baada ya kubadilisha rangi zao "mawaziri wa zamani Ali Benflis na Abdelmajid Tebboun walitangaza mnamo Alhamisi ugombeaji wao katika uchaguzi wa urais wa 12 Disemba" (Reuters 28/9/2019). Hawa na mfano wao ni sura za kutegemewa na nidhamu ya serikali na baadhi yao wanacheza dori ya upinzani. Ali Benflis, kiongozi wa chama cha National Liberation Front kinajiwasilisha kama chama cha kisiasa na kulingania mabadiliko. Kiongozi wake, Benflis alikuwa kiongozi wa serikali wa Bouteflika baina ya 2000 na 2003, ikimaanisha kuwa nidhamu hii inataka kuurudisha utawala ukiwa na sura mpya kidogo ikipendekeza kwamba watu wa Algeria wakubali uhadaifu na harakati (Hirak) ziishe!

3- Lakini, liko wazi kuwa harakati maarufu kwa upana wake zinazopinga uchaguzi chini ya utawala uliopo zina nguvu zaidi kuliko zile zinazounga mkono utawala au vile vinavyojiita vyama vya kisiasa ambavyo vinaunga mkono uchaguzi na hili linaifanya nchi kuelekea katika hali mbili zifuatazo:

- Ima utawala uliopo utalazimishwa kuhairisha uchaguzi katika dakika za mwisho kama ilivyokuwa tarehe ya uchaguzi ya 18/4/2019 na ulihairishwa.

- Au kutakuwa na uchaguzi ambao haukukamilika, hivyo basi harakati maarufu zitaendelea lau kama ambaye uchaguzi haukufanyika hata kama baadhi ya vikosi vitasusia harakati maarufu lakini hali zitakuwa nzuri kwa kuwepo kwa vurugu ili Mamlaka yaweze kusitisha harakati hizo baada ya kusema kwamba rais halali ashachaguliwa na kwamba maamuzi yake lazima yahishimiwe! Hivyo basi, mambo yanaendelea kuwa ya mshikemshike baina ya toa na uchukuwe!!

4- Hivyo basi, harakati zilizopo hazitoleta mabadiliko ya kweli

*Endelea Uk..16*

au ufufuaji ulio na ufanisi kwa sababu harakati hizi licha ya kuchipuza kimaumbile lakini uingiliaji kati wa Uingereza na Ufaransa ndani yake na makundi na wafuasi wanafanya harakati hizo kukosa ukamilifu hususan baada ya kuweka wazi mpangilio wa uongozi wa jeshi pamoja na utawala bali ni sehemu yake inayoipa maagizo na kuikataza. Hili linamaanisha kwamba mabadiliko yanaweza kupatikana tu ndani ya Algeria kwa kubadilisha utiifu wa jeshi kuwa ni Uislamu wa watu hawa sahihi. Hili linawezekana na kufaulu baada ya kuwaondosha majenerali wa juu, vibaraka wa Uingereza na Magharibi na kuwawezesha kundi la maafisa mukhilisina kuchukua udhibiti wa mambo ndani ya jeshi na kisha kunusuru mabadiliko ya kweli ambayo Ummah unayataka kwa msingi wa Uislamu.
Hili halimaanishi kuwa jeshi lishikilie serikali bali wawe watu wanaoinusuru kwa Ukweli ili uongozi wa kweli ambao Ummah unausubiri uweze kuleta mageuzi ya kina kwa kurudisha maisha ya Kiislamu na kusimamisha Khilafah Rashidah ya kweli ambayo itaufufua Ummah na kuifufua mimea na ziwa na turudi kupitia hiyo kama Mwenyezi Mungu alivyotutaka tuwe.

**{كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ}...**
“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.” [Al-i-Imran: 110]

**{وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * نَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ}**

“Na siku hiyo waumini watafurahi. Humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye Kurehemu.” [Ar-Rum: 4-5].

**4th Safar 1441 AH**
**03/10/2019 M**


Email: info@uqab.or.ke